*Jarida la Mwezi*

# TNMC HABARI

JARIDA TOLEO NO.03 | NOVEMBA 2023 | HALIUZWI

## Mhe. Ummy aagiza Daktari, Muuguzi Kuchukuliwa Hatua



- **Ni wale waliosababisha kifo cha Mjamzito Kituo cha Afya Kabuku, Wilaya ya Handeni Mkoani Tanga**

## YALIYOMO

**NDUNGILE: WATUMISHI ZINGATIENI MIIKO, MAADILI YA KAZI, JALINI WATEJA**

**WAUGUZI ,WAKUNGA MTWARA WANUFAIKA NA MAFUNZO YA MATUMIZI YA VYUMBA VYA UPASUAJI.**

**WAUGUZI, WAKUNGA WAHIMIZWA KUTUNZA SIRI ZA MTEJA**



*Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Yudas Ndungile, akifungua Kikao cha Kiutendaji kati ya Wauguzi, Wakunga, Wafamasia wa Mkoa wa Shinyanga*



## WAUGUZI, WAKUNGA MSITOE HUDUMA NJE YA MAWANDA YENU (SCOPE OF PRACTICE) – MSAJILI TNMC

# TIMU YA WAHARIRI

JARIDA MAALUMU BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

## MHARIRI MKUU

Bi.Agnes Mtawa

## MHARIRI

Mwakapiso Ndimmyake

## WARATIBU

Irene Chilewa na Rose Mhando

## MSANIFU JARIDA

Ezekiel M Nyalusi

P.O BOX1736 DODOMA
TEL.022-212133975 Fax.022-2133975 Mobile:0786785947

# Wauguzi, Wakunga Mtwara Wanufaika Mafunzo ya Matumizi ya Vyumba vya Upasuaji.

**Na Ezekiel Nyalusi.**

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limendelea kuwajengea uwezo Wauguzi na Wakunga Nchini kwa kuwafundisha jinsi ya kutoa huduma wanaposhiriki zoezi la upasuaji katika chumba cha upasuaji ili kuboresha huduma, Mafunzo hayo yamefanyika katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Ligula, Mkoani Mtwara.

Mafunzo hayo yaliwahusisha madaktari, wauguzi, wakunga pamoja na wahudumu wa Afya wapatao 97 kutoka chumba cha upasuaji, chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu, Idara ya kusafisha na kutakasa vifaa tiba, sehemu ya huduma za dharura, wodi ya Wazazi sambamba na wodi ya upasuaji kutoka Hospitali ya Rufaa ya Ligula na Hospitali ya Rufaa ya St.Benedict Ndanda zote za Mkoani Mtwara.

Akifafanua juu ya umuhimu wa mafunzo hayo Bi. Salome Kassanga, ambaye ni Muuguzi mtaalamu wa chumba cha upasuaji kutoka Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania amesema, mafunzo hayo yamefanyika chini ya uratibu wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kwa siku 14 yakiwa na alama 11.4 za mafunzo ya kujiendeleza kazini (CPD points) yakitumia moduli 06 katika usimamizi wa chumba cha upasuaji.

*“Kumekuwa na changamoto ambapo baadhi ya watumishi hawana ujuzi wa kutosha wa kusimamia na kuendesha huduma katika vyumba vya upasuaji hivyo, nia ya mafunzo haya ni kuwajengea uwezo ili kuzuia maambukizi kwa wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji”* amesema Bi. Kassanga.



***Bi. Salome Kassanga, ambaye ni Muuguzi mtaalamu wa chumba cha upasuaji kutoka Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania akitoa ufafanuzi kwa wauguzi na wakunga wakati wa mafunzo***

Hata hivyo, Bi. Kassanga, amewataka watumishi hao kuyafanyia kazi yale waliyojifunza ili kuhakikisha jamii ipate huduma iliyo bora na salama.

Kwa upande wake Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya St.Benedict Ndanda Dkt. Isaiah Sienz, amesema mafunzo hayo yamesaidia kuboresha mazingira ya vyumba vya upasuaji na kuwaongezea ujuzi watumishi hao ambapo hapo awali hawakuwa na ujuzi huo kutokana na kutosoma namna ya kutoa huduma ya aina hiyo, baada ya mafunzo kusitishwa hapa Nchini.

Pamoja na Mafunzo hayo Dkt. Sienz, amemshukuru Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kwa jitihada za utoaji wa mafunzo ya aina hiyo kwa watumishi waliopo kazini huku akiiomba serikali irudishe mafunzo hayo ili kuboresha utoaji wa huduma ya aina hiyo kwa wateja.

# Watumishi wa Afya Zingatieni Miiko, Weledi Maadili ya Kazi

**Na George Mganga**




***Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Yudas Ndungile, akifungua kikao kazi kati ya wauguzi na wakunga Mkoani wa Shinyanga***

Wauguzi, wakunga, Madaktari, na wafamasia Mkoani Shinyanga wameaswa kuzingatia miiko na Maadili ya kazi katika utumishi wao wanapo kuwa Hospitalini ili kuboresha huduma za Afya kwa kujali maslahi ya wagonjwa ambao ndiyo walengwa wakuu wanaopaswa kuhudumiwa.

Hayo yamesemwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Yudas Ndungile, wakati akifungua kikao kazi kati ya wauguzi, wakunga, Wafamasia wa Mkoa wa Shinyanga na Maofisa kutoka Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga.

Akifungua kikao kazi hicho kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga Dkt. Ndungile, amewataka watumishi katika Sekta ya Afya kuwa na lugha nzuri zenye staha kwa wateja.

*"Tuimarishe mawasiliano yetu na wateja, tuache ujuaji ambao hauna maana, hali ya sasa si kama ya zamani unaweza ukawa unakiuka maadili, kumbe mteja anakurekodi hata kukupiga picha bila wewe kujua kutokana na teknolojia ilivyo siku hizi tusijione kuwa sisi ni wataalamu zaidi kuzidi wagonjwa, siku hizi watu walioelimika ni wengi, hivyo tuongeze umakini kwa kuwajali na kutumia lugha nzuri ya Mawasiliano ili wateja wafarijike lakini pia waridhishwe na huduma zetu",* alisema. Dungile

Katika hatua nyingine, Dkt. Ndungile, ametilia mkazo kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Christina Mndeme, tabia ya kuacha matumizi ya simu (kuchati) wakati wa kumhudumia mteja kwa kueleza kuwa si busara sababu inaonesha dharau kwa wateja na badala yake akashauri kama mtumishi anataka kutumia simu, ni vema akamjulisha mteja wake kabla ya kuitumia.

Naye Afisa Maadili ambaye pia ni Mkunga Mbobezi kutoka Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, Bi. Mwajuma Mutabazi, amewasisitiza watumishi hao kuzingatia majukumu yao kadiri ya mwongozo wa viapo vyao vya kitaaluma, amesema kwa kufanya hivyo kutasaidia kutoa huduma nzuri kwa mteja sambamba na kufuata miiko na maadili ya kazi, ikiwa ni pamoja na kutumia lugha nzuri kwa mteja.

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia wanataaluma na taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria ya Mwaka 2010 na kanuni zake (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga Nchini ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

# Wauguzi, Wakunga Msitoe Huduma nje ya Mawanda yenu (Scope Of Practice) – Msajili TNMC

Na Ndimmyake Mwakapiso



*Wauguzi na wakunga wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti Mkoani Pwani wakifuatilia mafunzo ya Sheria na Maadili yanayotolewa na Msajili wa Baraza Bi.Agnes Mtawa, ambaye hayupo pichani.*

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Bi. Agnes Mtawa, ametoa rai kwa Wauguzi na Wakunga Nchini kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia taratibu za taaluma hiyo, ikiwa ni pamoja na uvaaji wa sare za kitaaluma zilizoidhinishwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga kwa mujibu wa Sheria, wakiwa katika maeneo ya kutolea huduma za Afya, kutoa huduma kwa kuzingatia mawanda ya taaluma( Scope of Practice) ,kutoa huduma zenye staha pamoja na kuheshimu mila na tamaduni za jamii husika.

Bi.Agnes Mtawa, ameyasema hayo, wakati akitoa Mafunzo ya Maadili, Sheria, Kanuni na taratibu za taaluma ya Uuguzi na Ukunga kwa wataalamu wa kada hiyo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti Mkoani Pwani.

Akifafanua suala la kufanya kazi ambazo si za taaluma hiyo, amesema, kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wauguzi na wakunga, kufanya kazi tofauti na zile zinazoruhusiwa kitaaluma kama vile huduma ya upasuaji na kuwataka waache tabia ya kutoa huduma ambazo ni nje ya mawanda yao,na wanapokutana na wagonjwa wanaohitaji huduma hizo basi wahakikishe wanatoa rufaa kwa wataalamu husika.

*"Kwa hiyo nawakumbusha kufanya kazi zilizo ndani ya mawanda yenu (scope of practice) msifanye mambo kwa kukariri kwamba mimi hiki nakijua, mbona mimi naonaga wanavyofanya hivi,mfano ni upasuaji mkubwa."* alisema Bi.Mtawa

Baraza la Uuguzi na Ukunga Nchini, limekuwa na uratibu wa kufanya ziara katika Mikoa mbalimbali na wilaya zake Nchini kwa lengo la kuwakumbusha wauguzi na wakunga maadili na Sheria za taaluma ya Uuguzi na Ukunga ili waweze kutoa huduma bora na salama kwa wateja wanaowahudumia.

# “Zingatieni Mafunzo kwa Vitendo” - Bi. Masenga

Na Ndimmyake Mwakapiso



***Mkurugenzi wa Mafunzo na maendeleo ya taaluma wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Happy Masenga, alikizungumza na kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma cha Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Jijini Dodoma.***

Wanafunzi wanaosoma taaluma ya Uuguzi na Ukunga katika vyuo mbalimbali Nchini, wameshauriwa kuzingatia Mafunzo kwa vitendo wanapokuwa vyuoni ili kuwa na umahiri unaotakiwa katika taaluma ya Uuguzi na Ukunga.

Kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Mafunzo na maendeleo ya taaluma wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Happy Masenga, alipozungumza na kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma cha Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Jijini Dodoma.

*“Ninawashauri Wanafunzi waliopo vyuoni wanaosoma taaluma ya Uuguzi na Ukunga kwamba, wanapokuwa katika Mafunzo wazingatie sana kujifunza kwa vitendo wanapokuwa katika Hospitali mbalimbali kwa mafunzo ya vitendo, hii inamsaidia sana kuimarisha weledi wao na umahiri unaotakiwa katika utoaji huduma, hii itapelekea kufanya vizuri katika mitihani ya usajili na leseni”* amesema Bi. Masenga

Akizungumzia kuhusu vyuo vya Uuguzi na Ukunga vilivyosajiliwa kuendesha Mafunzo Nchini, Bi. Masenga, amevitaka vyuo hivyo kuendesha Mafunzo kwa kuzingatia mitaala sambamba na kuwafuatilia wanafunzi wao wanapokuwa katika maeneo ya kujifunza kwa vitendo ili kutoa wauguzi wenye ubora na umahiri unaotakiwa.

Katika hatua nyingine Bi. Masenga, amebainisha ratiba ya kufanyika kwa mitihani ya usajili na leseni, kwamba hufanyika kwa awamu tatu katika kila Mwaka wa fedha ambapo ni Mwezi Agosti, Disemba na Aprili.

Pia amewashauri watahiniwa wote wanaotarajia kufanya Mtihani wa Usajili na Leseni mwezi Disemba 2023, kuchagua vituo vilivyo karibu na Mikoa wanayoishi, amevitaja vituo hivyo kuwa ni pamoja na Taasisi ya Afya na Sayansi Shirikishi Tandabui-(Mwanza),
Chuo Kikuu cha Kampala-(Dar es Salamu),
Chuo cha St. John-(Dodoma),
Chuo cha Stephano Moshi-(Kilimanjaro),
Chuo cha Afya na Sayansi shiriki-Mbalizi(Mbeya),
Chuo Kikuu cha Katoliki-Iringa (RUCU) Pamoja na
Tabora Polytechnic-(Tabora.)

# Wauguzi, Wakunga Wahimizwa kutunza Siri za Mteja

Na Ezekiel Nyalusi



*Mkurugenzi wa Leseni na Maadili kutoka Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Jane Mazigo wa kwanza kushoto, katika picha ya pamoja baada ya Mafunzo kwa wauguzi na wakunga katika Halmashauri ya Chalinze*

Mkurugenzi wa Usajili, leseni na Maadili kutoka Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Jane Mazigo, ametoa Mafunzo kwa wauguzi na wakunga katika Halmashauri ya Chalinze ikiwa ni lengo la kuwakumbusha watumishi hao kuzingatia Sheria, Kanuni pamoja na Maadili katika utoaji wa huduma kwa wateja katika vituo Afya.

Akizungumza Novemba 15, 2023 katika Ukumbi wa Kikwete Halmashauri ya Chalinze amesema, katika utoaji wa huduma kwa wagonjwa ni vizuri kuzingatia usiri katika taarifa tunazozipata kwa mteja ikiwa ni pamoja na kuwajibika kwa vitendo katika maeneo ya kazi, uadilifu na kutumia rasilimali zilizopo kwa usahihi ili kuepuka migogoro.

Ameongeza kuwa, watumishi wanapaswa kuzingatia usawa katika utoaji wa huduma pasipo upendeleo wala ubaguzi pamoja na kuhakikisha wanatunza vifaa vya dharura ili wagonjwa wanapofika katika vituo wapate huduma kwa haraka.

Aidha amewaasa kuwa na tabia ya kuheshimiana, kujitambua na kushirikiana katika utoaji wa taarifa sahihi ili jamii iweze kuwa salama.

Katika hatua nyingine Bi. Mazigo, ametoa wito kwa wauguzi na wakunga kujiendeleza kitaaluma kwa kuwa sekta ya Afya huenda na mabadiliko.

Kwa upande wake Muuguzi Mkuu wa Halmashauri ya Chalinze Bi. Gabriela Mtwale, amesema mafunzo hayo yatapunguza malalamiko kwenye baadhi ya vituo vya Afya huku akitoa rai kwa watumishi hao kuacha kutumia simu wakati wa utoaji huduma kwa wateja na kuhakikisha wanatumia vikao vyao vya kila robo, kukumbushana na kuelezana namna bora ya utoaji huduma unaozingatia Maadili.

Hata hivyo, wauguzi na wakunga wa Halmashauri ya Chalinze, wamelishukuru Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kwa Mafunzo hayo kwa kuwakumbusha kufanya kazi kwa weledi kwa kuzingatia miongozo, taratibu, Sheria na kanuni huku wakiomba Mafunzo hayo yawe endelevu kwani yatawasaidia kutoa huduma bora kwa jamii.

# Muuguzi, Mkunga Ukitoa Huduma Bila Leseni utakabiliwa, kifungo cha Miaka Mitano, Faini.

Na Ndimmyake Mwakapiso



***Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Agnes Mtawa, akitoa Elimu ya Sheria na Maadili ya Uuguzi na Ukunga Wilayani Mafia, Mkoani Pwani.***

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Agnes Mtawa, amewataka wauguzi na wakunga Nchi, kutekeleza Sheria inayowataka kuwa na leseni hai ya kutolea huduma ili wawe na uhalali wa kuwahudumia wateja waonafika kwenye Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati wanazofanyia kazi, sambamba na kutambulika kama wataalamu wa tasnia hiyo.

Bi. Mtawa, ametoa maelekezo hayo Wilayani Mafia, Mkoani Pwani, wakati akitoa Elimu za Sheria na Maadili ya taaluma ya Uuguzi na Ukunga, ikiwa ni muendelezo wa ziara za Baraza katika Mkoa wa Pwani na Wilaya zake.

Amesema suala la Muuguzi na Mkunga kuwa na leseni hai ili uruhusiwe kutoa huduma, kwa mteja sio jambo la hiari au matakwa ya Msajili wa Baraza, bali linatokana na Sheria halali ya Uuguzi na Ukunga iliyotungwa Mwaka 2010 ili kuhakikisha huduma zinazotolewa ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

*"Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010, Kifungu cha (38)(i)(a)(c) imeanisha hapa, kwamba Muuguzi au Mkunga yeyote, atakapo patikana anatoa huduma bila kuwa na lesini hai, adhabu zake ni kifungo cha miaka 05 au faini isiyopungua shilingi Milioni moja (1,000,000 au isiyozidi millionI tatu ( 3,000,000) au vyote kwa Pamoja, aidha, kifungu cha (44) kimeainisha mwajiri ambaye kwa makusudi kabisa atamuajiri au kufanya kazi na muuguzi asiye na leseni hai chini ya mamlaka yake ikithibitika adhabu yake ni faini isiyopungua Sh.Milioni moja (1,000,000) au kifungo kisichopungua miezi sita"* alisema Bi.Mtawa

Akisisitiza kuhusu umuhimu wa kila muuguzi na mkunga kuwa na leseni hai Bi. Mtawa, ametanabaisha kuwa, mtu yeyote atakayebainika kutokuhuisha leseni yake miezi sita tangu ilipoisha muda wake kwa mujibu wa kanuni ya Usajili, uorodheshwaji na leseni kifungu cha (8)(a)(b)(c) Msajili amepewa Mamlaka ya kumfuta katika daftari la usajili na kutoa taarifa kwenye mamlaka yake ya Ajira.

# Mhe. Ummy aagiza Daktari na Muuguzi kuchukuliwa hatua

**Na Mwandishi wetu**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu , ameyaagiza Mabaraza ya madaktari na wauguzi kuwachukulia hatua Mganga na Muuguzi waliosababisha kifo cha mjamzito Mariam Zahoro, kilichotokea Kituo cha Afya Kabuku, Wilaya ya Handeni Mkoani Tanga.

Mwalimu amesema, Mariam, hakufariki kwa ajili ya kukosa kiasi cha shilingi 150,000, bali ni kwa ajili ya uzembe wa baadhi ya wahudumu wa Afya kwa kushindwa kuwajibika kutokana na hali aliyokuwa nayo mgonjwa.

Ameyasema hayo Novemba 27, 2023 baada ya kupokea taarifa ya Tume iliyoundwa kuchunguza jambo hilo lililotokea Novemba 11, mwaka huu, kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Kituo cha Afya Kabuku, ambapo Tume imebaini wahudumu wawili ndiyo wenye makosa.

*“Tunataka Mabaraza ya Madaktari na Wauguzi wachukue hatua kwa Daktari na Muuguzi walioshindwa kuwajibika, kosa la Daktari ni kushindwa kufika kwa wakati akiwa ameelezwa hali ya mjamzito ni mbaya, hata alipofika, alishindwa kuchukua hatua ya kumpeleka Hospitali ya Wilaya ya Handeni, Mkata baada ya kumkosa Muuguzi wa dawa za usingizi ili mgonjwa afanyiwe upasuaji lazima apewe dawa za usingizi,”* ameeleza Mhe.Mwalimu na kuongeza kuwa

*“Kosa la Muuguzi ni kumueleza mgonjwa kuwa anatakiwa alipe 150,000 wakati huo sio utaratibu, kwani alitakiwa atoe huduma bila kudai fedha hizo, hivyo, nitangaze kwamba mjamzito hakupoteza maisha kwa ajili ya kukosa sh.150,000, bali ni kwa ajili ya uzembe wa baadhi ya wahudumu wa Afya,”*



***Waziri wa Mhe. Afya Ummy Mwalimu, akizungumza kwenye Mkutano wa hadhara uliofanyika Kituo cha Afya Kabuku.***

Mwalimu amesema Sera ya Afya ya mwaka 2007 inamtaka mjamzito kupata huduma bila malipo, hivyo amepinga makubaliano yaliyofikiwa kwenye kata kati ya wahudumu wa Afya na watendaji akiwemo Diwani wa eneo hilo kupitisha kuwa mjamzito atatoa sh. 150,000 kwa ajili ya upasuaji.

Amesema anataka Mabaraza hayo yatoe maamuzi ndani ya wiki mbili, huku akiwaahidi Wananchi hao kuwa wahudumu hao wawili hawatarudi Kabuku na kutaka hatua kali zichukuliwe dhidi yao iwe onyo kwa wengine.

Hata hivyo Waziri wa Afya Ummy Mwalimu , amekiri baadhi ya majengo kwenye kituo hicho yamechoka, na atatafuta fedha kujenga mengine.

*Credit:Gazeti la Majira*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA**

# TANGAZO
# MTIHANI WA USAJILI NA LESENI DESEMBA, 2023

Wahitimu wote mnatangaziwa kuwa mtihani wa Usajili na Leseni utafanyika tarehe 29/12/2023, maombi yanafanyika kupitia mtandao kwa kutumia mfumo wa Baraza ***https://tnmcis.tnmc.go.tz/*** kuanzia tarehe 6/11/2023 hadi tarehe 20/12/2023. Kila muombaji atatakiwa kujisajili na kulipia kiasi cha Shilingi 150,000/- ,kwa wale wanaoomba kufanya mtihani huu kwa mara ya kwanza na Shilingi 75,000/= kwa wanaorudia.

Waombaji wanaotarajia kufanya Mtihani huu kwa mara ya kwanza, wanatakiwa kuhakikisha wamefanya usajili wa awali (Indexing) kwa mujibu wa kifungu cha 14 (1) cha kanuni za mafunzo. Pia, kuzingatia taratibu zote za maombi ambazo zimeambatanishwa ikiwa ni pamoja na kuweka picha sahihi (Passport Size), kujaza majina sahihi yanayoendana na vyeti vya kufuzu sekondari, kufanya malipo kwa wakati na kuchagua kituo sahihi cha mtihani kati ya vilivyoorodheshwa katika jedwali hapa chini:

| KITUO CHA MTIHANI | MKOA | IDADI |
|---|---|---|
| TAASISI YA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI - TANDABUI | MWANZA | 1000 |
| CHUO KIKUU CHA KAMPALA | DSM | 1000 |
| CHUO KIKUU CHA ST.JOHN | DODOMA | 800 |
| CHUO CHA STEPHAN MOSHI-KILIMANJARO | MOSHI | 800 |
| CHUO CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI -MBALIZI | MBEYA | 800 |
| CHUO KIKUU CHA KATOLIKI RUAHA (RUCU) | IRINGA | 700 |
| TABORA POLYTECHNIC | TABORA | 700 |

***@tnmchabari*** ***www.tnmc.go.tz***






# TANZIA

Baraza la Uuguzi na Ukunga limepokea kwa masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele za haki, baada ya kumaliza kazi yao hapa duniani; Mwenyezi Mungu azipokee Roho zao.

1.Marehemu Tabitha Nkane, alifariki tarehe 13/11/2023 alikuwa akifanya kazi Zahanati ya sabasaba - Mkoani IRINGA

2.Marehemu Secilia Kumburu, alifariki 16.11.2023, alikuwa akifanya kazi kituo cha afya, Dumila-KILOSA

3.Marehemu lina james Mbwambo, alifariki 24.11.2023 alikuwa akifanya kazi Serengeti DC- Mkoani MARA.

4.Marehemu Benadetha Masolwa, alifariki 24.11.2023 alikuwa akifanya kazi Bunda DC- Mkoani MARA

5.Marehemu Josephat jabir Ally, alifariki 28.11.2023 alikuwa akifanya kazi Zahanati ya Kindimba Chini-Mbinga.

6.Marehemu Fedrick Orsa, alifariki 29.11.2023. alikuwa akifanya kazi Hospitali ya Peramiho- Mkoani RUVUMA.

***WAPUMZIKE KWA AMANI***

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA**

# TANGAZO:

## YAH: WANAFUNZI WOTE WALIOLIPIA INDEXING NJE YA MFUMO.

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania linapenda kuwajulisha wanafunzi wote waliolipia Usajili wa awali (*student Indexing*) nje ya Mfumo wanaweza kuendela kufanya maombi yao ya Mtihani pasipo kulipia Usajili wa awali (*student Indexing*) kama mfumo ulivyowataka hapo awali.

Kwa yeyote atakayepata changamoto atoe taarifa kwa kupiga simu zilizopo katika mfumo wa Baraza ***(hppts://ww.tnmcis.go.tz).***

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia Wanataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria ya Mwaka 2010 na kanuni zake ***(The Nursing and Midwifery Act, 2010)*** ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga Nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

Imetolewa na:

**IDARA YA HABARI NA UHUSIANO**
**BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA.**

***26 /11/2023.***

JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA TOLEO NO 03

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
P.O BOX1736 DODOMA ,TEL.022-212133975
Fax.022-2133975,Email:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI  ZOTE ZIMEHIFADHIWA